

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS - TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA NKASI



**TANGAZO KWA UMMA KUHUSU MIKOPO INAYOTOLEWA KWA VIKUNDI VYA WANAWAKE, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAMU.**

**(Limetolewa Kwa kuzingatia Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa (Sura ya 290) na Kanuni zilizotengenezwa chini ya Kifungu cha 37A (4) juu ya utoaji na Usimamizi wa Mikopo kwa Vikundi Vya Wanawake, Vijana na wenye Ulemavu)**

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Nkasi anatangaza uwepo wa fedha kwa ajili ya kuvikopesha vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu, ambapo jumla ya Shilingi 300,000,000 /= zimetengwa katika robo ya Nne ya mwaka wa fedha 2024/2025. Hivyo, Vikundi vyenye sifa vinakaribishwa kuleta maombi katika Ofisi za Serikali za mitaa zilizopo katika maeneo yenu.

Vikundi vinavyotakiwa kuomba mikopo vinapaswa kuwa na sifa zifuatazo: -

- (i) Kikundi cha wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kilichotambuliwa na kupewa cheti cha utambuzi na halmashauri,
- (ii) Kikundi kiwe kinachojishughulisha na shughuli za ujasiriamali mdogo au wa kati au kikundi kinachotarajia kuanzisha shughuli za ujasiriamali,
- (iii) Kikundi cha wanawake na vijana kiwe na idadi ya wanakikundi kuanzia watano (5) na kuendelea na kikundi cha watu wenye ulemavu kiwe na wanakikundi wasiopungua wawili (2). Pia kwa kuzingatia Kanuni ya 7(1) Bila kujali masharti ya kanuni ya 6 mtu mwenye ulemavu anaweza kuwa na sifa ya kupata mkopo kama kikundi cha watu wenye ulemavu endapo,
  - (a) Timu ya Menejimenti ya Halmashauri itajiridhisha kuwa amekosa mtu mwingine mwenye ulemavu na sifa ya kua mwanakikundi wa kikundi cha watu wenye ulemavu.

- (b) Anajishughulisha na ujasiriamali au anakusudia kuanzisha shughuli za ujasiriamali mdogo au wa kati.
- (c) Ana akaunti ya benki iliyofunguliwa kwa jina lake kwa shughuli maalumu za kiujasiriamali na,
- (d) Hana ajira rasmi.
- (iv) Kikundi kiwe na akaunti ya benki iliyofunguliwa kwa jina la kikundi kwa ajili ya matumizi ya shughuli za kiujasiriamali; na
- (v) Wanakikundi lazima wawe ni raia wa Tanzania wasio na ajira rasmi, wenye akili timamu na wenye umri wa kuanzia miaka 18 na kuendelea. Aidha, kikundi cha vijana kitapaswa kuwa na wanakikundi wenye umri kuanzia miaka 18 hadi 45.

Maombi yote yatumwe kupitia mfumo wa kielektroniki (**tembelea tovuti: mikopohalmashauri.tamisemi.go.tz**) ili kutambuliwa na kuomba mkopo au wasiliana na Afisa Maendeleo ya Jamii wa kata husika au Mtendaji wa Kata husika.

Kikundi kinachoomba mkopo kinapaswa kuwa na viambatisho vifuatavyo; barua ya kikundi ya kuomba mkopo iliyopitishwa na Afisa Mtendaji wa Kijiji/Mtaa, Muhtasari wa kikundi wa kuomba mkopo, andiko rahisi la mradi unaoombewa mkopo kwa kuzingatia fomu iliyo ndani ya mfumo na taarifa ya akaunti ya benki.

Mwisho wa kuwasilisha maombi ni tarehe 02 mwezi Mei mwaka 2025

Tangazo hili limerolewa na: -



.....  
**Afraha N. Hassan**  
**Mkurugenzi Mtendaji (W)**  
**Nkasi**

MKURUGENZI MTENDAJI  
MIL MASHAURI YA WILAYA  
NKASI